NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

Ridván 2015

Kwa Wabahá'í wa Ulimwengu

Marafiki wapendwa sana,

Msimu ung'aao wa Ridván unakaribia, na kutoka vilele ambavyo jumuiya ya Jina Kuu Kabisa imevifikia, matarajio yenye matumaini huonekana upeoni. Mandhari kubwa mno imepitiwa: mipango mipya ya ukuaji imejitokeza, na wakati mamia zaidi hata hivyo sharti iibuke katika miezi kumi na mbili ijayo, juhudi kuanzisha mtindo utakiwao wa shughuli tayari zimeanza karibu katika kila mojawapo ya klasta zihitajiwazo kufikia zile 5000 zihitajiwazo katika Mpango wa Miaka Mitano. Mipango iliyopo inaimarika, mingi ikionesha kwa udhahiri zaidi ni kitu gani humaanishwa kwa Hoja ya Mungu kuenea zaidi kwenye mandhari ya kijamii pande zote za klasta na ndani ya ujirani au kijiji.Njia zielekezazo kwenye upanuzi mkubwa ulio imarika na uimarishaji zinafuatiliwa kwa hatua zilizo thabiti zaidi,mara nyingi vijana jasiri wakiongoza njia. Njia ambazo kwamo nguvu za ujengaji jamii za Imani zinaweza kupata kufunguliwa katika mazingira mbali mbali zinaanza kuonekana wazi zaidi, na zile sifa bainifu ambazo lazima zije kuainisha ukunjukaji zaidi wa mchakato wa ukuaji katika klasta zinaanza kuonekana kidogo kidogo.

Mwito wa kutekeleza na kusaidia kazi hii huelekezwa kwa kila mfuasi wa Baha'u'lláh, na utaamsha mwitikio katika kila moyo ambao huumizwa kwa ile hali duni ya ulimwengu, hali isikitishayo ambamo kutoka humo watu wengi mno wanashindwa kupata nafuu. Kwa kuwa, hatimaye, ni utendaji wa kiutaratibu, uliodhamiriwa, na usio na nafsi ufanywao ndani ya kumbatio pana la mfumo wa Mpango ambao ndio mwitikio jenzi kabisa wa kila muumini anayejali kwa magonjwa yanayo ongezeka ya jamii isiyo na utaratibu. Katika mwaka uliopita, imedhihirika zaidi tena kwamba, katika mataifa mbali mbali katika namna mbali mbali, ule muafaka wa kijamii uzunguukao mawazo bora ambayo kimila yameunganisha na kufungamanisha pamoja watu umechakaa na umekwisha. Hauwezi tena kutoa kinga ya kuaminika dhidi ya nadharia mbali mbali zijinufaishazo, zisizo vumilivu, na zenye sumu ambazo hujilisha utovu wa ridhaa na chuki. Pamoja na ulimwengu usio kubaliana unaojitokeza kila siku upungukiwao kujiamini, watetezi wa kanuni hizi haribifu huwa jasiri na wasio na aibu. Tunakumbuka hukumu dhahiri kutoka Kalamu Kuu: "Wao wako hima kuelekea Moto wa Jehanamu, na huudhania kuwa mwangaza." Viongozi wenye nia safi wa mataifa na watu wema wameachwa wakihangaika kukarabati mipasuko iliyo dhahiri katika jamii na wakishindwa kuzuia kuenea kwao. Matokeo ya yote haya sio tu ya kuonekana katika ugomvi wa papo hapo au uangamiaji katika utaratibu. Katika tuhuma ambayo humpambanisha jirani dhidi ya jirani na kukata mafundo ya ukoo katika uhasama wa mengi mno wa yale yaonekanayo kukubalika kama mazungumzo ya kijamii, katika urahisi ambao kwao matamanio kwa hamasa za aibu za kibinadamu hutumiwa ili kupata mamlaka na kulundika mali –

katika yote haya kuna ishara zilizo dhahiri kwamba ile nguvu ya kimaadili ambayo hudumisha jamii imemalizwa vibaya sana.

Lakini kuna uhakika katika ufahamu kwamba, kati ya uchangukaji huu, aina mpya ya maisha ya pamoja inajitokeza ambayo hujidhihirisha kivitendo kwa yote yale yaliyo ya mbinguni ndani mwa binadamu. Tumeona jinsi, hasa katika mahali mule ambapo nguvu katika ufundishaji na shughuli za ujengaji jamii imedumishwa, marafiki wameweza kujilinda wenyewe dhidi ya nguvu za mambo ya kiulimwengu ambayo huhatarisha udhoofishaji nguvu zao zenye thamani. Sio tu hilo, lakini katika mambo yote yale mengine yanayo hitaji muda wao, kamwe hawasahau yale yalio matakatifu na kazi muhimu mbele yao. Uangalifu kama huo kwa mahitaji ya Imani na kwa maslahi bora kabisa ya binadamu huhitajika katika kila jamii. Mahali ambapo mpango wa ukuaji umeanzishwa katika klasta ambayo haijafunguliwa hapo awali, tunaona jinsi mishtuko ya mwanzo wa shughuli iibukayo kutokana na upendo kwa ajili ya Baha'u'lláh uliomo katika moyo wa muumini aliyejifunga. Licha ya ugumu wa mipango ambayo hatimaye sharti iingizwe kadiri jamii ikuavyo katika ukubwa, shughuli yote huanza kwa uzi wa kawaida wa upendo. Ni uzi muhimu ambao kutoka kwake umefumwa mtindo wa juhudi yenye subira na juhudi za pamoja, duru baada ya duru, kuwafahamisha watoto wadogo, vijana, na watu wazima mawazo ya kiroho, kukuza hisia kwa ajili ya ibada kupitia mikusanyiko kwa ajili ya sala na ibada; kuamsha mazungumzo ambayo huangazia ufahamu, kuanzisha idadi ziongezekazo daima juu ya ujifunzaji wa maisha wa neno la Uumbaji na kutafsiriwa kwake katika vitendo; kukuza pamoja na wengine, uwezo kwa ajili ya huduma; na kusindikizana katika zoezi la kile kilichoshikwa. Marafiki wapendwa sana, wapendwa wa Uzuri wa Abha: Tunawaombea nyinyi kwa dhati kila wakati tunapojiwasilisha wenyewe kwenye Kizingiti kitakatifu Chake, kwamba upendo wenu Kwake uweze kuwapa nguvu kuweka wakfu maisha yenu kwa Hoja Yake.

Umaizi mwingi uibukao kutoka klasta, na kutoka vituo vya shughuli ya nguvu ndani mwao, ambapo nguvu za maisha ya jamii zimejumuisha idadi kubwa za watu hustahili kutajwa kwa namna ya kipekee. Tumefurahishwa kuona jinsi utamaduni wa kusaidiana, uliowekwa juu ya msingi wa urafiki na huduma nyenyekevu, umejiimarisha wenyewe kikawaida kabisa katika makazi kama hayo, ukiwezesha roho zaidi na zaidi kuletwa kiutaratibu ndani ya uzio wa shughuli za jamii. Naam, katika idadi iongezekayo ya mazingira mwenendo wa watu kuelekea muono wa Baha'u'lláh kwa ajili ya jamii mpya hauonekani tena kama matarajio yavutiayo lakini kama uhalisi unaoibuka.

Tungependa kuwaambia maneno machache zaidi wale walio miongoni mwenu ambao ndani ya mazingira yao maendeleo ya kuonekana bado hayajatukia na ambao hutamani sana badiliko. Muwe na matumaini. Haitakuwa hivyo wakati wote. Je, historia ya Imani yetu haijajawa simulizi za mianzo yenye nuksi lakini matokeo ya ajabu? Ni mara ngapi matendo ya waumini wachache – vijana au wazee – au ya ukoo mmoja, au hata ya roho iliyo pweke, wakati imedhibitishwa na nguvu ya msaada mtakatifu, imefanikiwa katika ukuzaji jamii za mtikiso katika hali za nchi zionekanazo

zisizo kalika? Msidhanie kwamba suala lenu kiasili ni tofauti. Badiliko katika klasta, likiwa haraka au lilipatikana kwa kazi ngumu, halitiririki wala kutoka njia ya kifyomula wala kutoka shughuli ya kubahatisha; hujitokeza kwa mdundo wa utendaji, tafakari, na ushauriano, na husukumwa na mipango ambayo ni matokeo ya uzoefu. Mbele ya haya, na chochote kiwacho matokeo yake ya mara moja, huduma kwa Mpendwa, yenyewe, ni chanzo cha furaha inayodumu kwa roho. Jipeni moyo, pia, kutokana na mfano wa ndugu zenu wa kiroho katika Chanzo cha Imani, jinsi msimamo jenzi wao, unyumbukaji wao kama jamii, na uthabiti wao katika ukuzaji wa Neno la Mungu vinaleta badiliko katika jamii yao kwenye ngazi ya fikra na matendo. Mungu yu pamoja nanyi, yu pamoja na kila mmoja wenu. Katika miezi kumi na mbili ambayo imebakia ya Mpango, acha kila jamii iendelee mbele kutoka hali yake ya sasa hadi iliyo imara zaidi.

Kazi ya umuhimu kabisa ya upanuzi na uimarishaji huweka msingi imara kwa ajili ya jitihada ambazo ulimwengu wa Kibaha'i unatakiwa kuzifanya katika maeneo mengine mengi. Kwenye Makao Makuu ya Kibaha'i ya Ulimwengu, jitihada zinaongezeka kuingiza katika katalogi na faharasa maudhui ya maelfu ya nyaraka ambayo hufanya ule urithi wa thamani kubwa mno, Maandiko Matakatifu ya Imani yetu, uliokabidhiwa kwa ajili ya manufaa ya binadamu wote – hii, ili kuchapuza uchapishaji wa vitabu vya Maandiko, katika lugha zao za asili na katika tafsiri ya Kiingereza pia. Jitihada kuanzisha Mashriqu'l-Adhkar nane, Mahekalu matakatifu yaliyoinuliwa kwa utukufu wa Mungu, zinaendelea kwa haraka. Kazi ya mambo ya nje kwenye ngazi ya kitaifa imefanikiwa kwa udhahiri na imeongezeka kuwa ya kiutaratibu, zaidi ilipoamshwa na utoaji wa waraka, uliotumwa kwa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa miezi sita iliyopita, ambao hutumia uzoefu mwingi uliofanyizwa katika muda wa miongo miwili iliyopita na hutoa mfumo uliotanuliwa kwa ajili ya ukuzaji wa jitihada hizi siku zijazo. Wakati huo huo, Ofisi mbili mpya za Jumuiya ya Baha'i ya Kimataifa, wenzi kwa Ofisi yake ya Ofisi ya Umoja wa Mataifa iliyoko New York na Geneva na kwa Ofisi yake huko Brussels, zimefunguliwa huko Addis Ababa na Jakarta, kupanua fursa kwa ajili ya taswira za Hoja kutolewa kwenye ngazi ya kimataifa huko Afrika na mashariki ya kusini mwa Asia. Mara nyingi yakishawishiwa na mahitaji ya ukuaji, safu ya Mabaraza ya Kitaifa yanajijengea uwezo wao wa kiutawala, uonekanao katika usimamizi wao wa uangalifu wa raslimali walizo nazo, jitihada zao kufahamu kwa undani hali za jamii zao, na kuwa macho kwao katika kuhakikisha kwamba utendaji kazi wa Ofisi zao za Kitaifa daima huimarika zaidi; haja ya kuweka katika utaratibu jumla ivutiayo ya maarifa yajilimbikizayo hivi sasa katika eneo hili imeongoza kwenye uundwaji wa Ofisi huko Makao Makuu kwa ajili ya Maendeleo ya Mifumo ya Kiutawala. Ari kwa ajili ya utendaji wa kijamii za aina mbali mbali huendelea kuongezeka katika nchi nyingi, zikiwezesha mengi kushikwa juu ya jinsi hekima iliyohifadhiwa katika Mafundisho inavyoweza kutumiwa kuboresha hali za kijamii na kiuchumi; uwanja huu ni wa matumaini mno kwamba tumeanzisha Halmashauri ya ushauri ya Kimataifa ya wajumbe saba kwa Ofisi ya Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi, kuanzisha hatua ifuatayo katika ukuaji pole pole wa Ofisi hiyo. Wajumbe watatu wa Halmashauri hiyo watahudumia pia kama kikundi cha uratibu cha Ofisi na watakuwa wanaishi katika Nchi Takatifu.

Kwenye Ridván hii, basi wakati tunaona mengi ya kufanywa, tunawaona wengi walio tayari kukifanya. Katika maelfu ya klasta, ujirani, na vijiji, michipuko mipya ya imani na hakika hububujika, ikichangamsha roho za wale ambao wameguswa na maji yao yanayo huisha. Katika mahali fulani, mtiririko ni kijito imara, katika baadhi, tayari ni mto. Sasa sio wakati kwa roho yeyote kukawia ukingoni- acha wote walikubali wimbi lisongalo mbele.

*Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.*